

# KIFUA KIKUU (TB)

## Matibabu ya kikohozi katika famasia

### Dalili za maambukizi ya msingi ya kifua kikuu



Homa



Kupungua uzito




Kukohoa damu



Kupoteza hamu ya kula



Jasho la usiku



Uchovu


## FANYA



Uliza kila mtu aliye na kikohozi kuhusu muda ambao amekua na kikohozi na dalili zingine zozote.



Kama kikohozi kimeendelea kwa muda wa wiki mbili au zaidi, shuku kifua kikuu.



Tuma wanaoshukiwa kuwa na kifua kikuu kwa kituo cha afya kilicho karibu au kwa mtaalamu wa kibinafsi aliyehitimu kufanyiwa vipimo vya uchunguzi wa TB.



## USIFANYE

### USIPEANE

Viuvijasumu kama fluoroquinolones (kwa mfano; ciprofloxacin, levofloxacin) ama steroids (kwa mfano; dexamethasone, betamethasone) bila pendekezo halali kutoka kwa mtaalamu wa afya.

### USIPEANE

dawa za kifu kikuu kama rifampicin, ethambutol, isoniazid, pyrazinamide bila pendekezo halali kutoka kwa mtaalamu wa afya.



## Misaada ya dalili

Ni sawa kupeana dawa za kupeana nafuu ya muda kama paracetamol na dawa za kikohozi.

**Onyo:** Usipeane dawa za kukandamiza kikohozi zinazoweza kuficha dalili za kifua kikuu.

# 4.1

## MILIONI

### IDADI YA WATU DUNIANI WENYE KIFUA KIKUU WASIOJULIKANA



Kwa kawaida, wafamasia ni wahudumu wa kwanza ambao huwasiliana na wagonjwa. Kwa hivyo, wana jukumu muhimu la kusuluhisha shida hii.



Supported by

